

Ni jinsi gani ambavyo madereva wa magari makubwa na wanakijiji wa Tanzania wanavyofikiria juu ya kujamiiana kinyume na maumbile

Lengo la utafiti

Kudadisi ufahamu wa madereva wa magari makubwa ya mizigo na wanakijiji kutoka Tanzania juu ya kujamiiana kinyume na maumbile na madhara yake kiafya.

Namna kazi/utafiti ulivyofanyika

Utafiti huu ulijumuisha mahojiano na madereva wa magari makubwa ya mizigo kwa kupitia hojaji nane (8) za kina kwa njia ya mtu mmoja mmoja. Pia majadiliano ya vikundi viwili (2) yanayo jumuisha madereva wa magari makubwa ya mizigo yalifanyika. Na kwa upande wa wanavijiji kulikuwa na hojaji kumi na sita (16) na majadiliano ya vikundi manne (4).

Hivyo, washiriki katika utafiti huu ulishusisha wanawake ishirini na nne (24) na wanaume arobaini na sita (46). Mnyambulisho wa taarifa zilizokusanywa katika utafiti huu ulifanyika kwa kuangalia mambo mbali mabali yaliyojitokeza katiak mada kwa kupitia njia za kitafiti za kunyambulisha taarifa.

Matokeo ya utafiti

Sababu zinasowanya wanaume wapendeleo kufanya mapenzi kinyume na maumbile ni pamoja na msongo wa mapenzi, imani kuwa kufanya mapenzi kinyume na maumbile ni salama zaidi, ni njia mbadala wa kufanya mapenzi, udadisi na kuhakikisha kwamba yeye ni mwanaume na anaweza.

Kwa upande wa wanawake sababu za kufanya mapenzi kinyume na maumbile ni pamoja na hitaji la fedha, kumshika mwenza, njia mbadala ya kufanya mapenzi wakati wa hedhi, kuzuia mimba na imani kuwa kufanya mapenzi kinyume na maumbile kunakuza maumbile. kwani inaaminika kuwa kufanya mapenzi kinyume na maumbile inaongeza ukubwa wa matakao. Washiriki waliowengi wanaamini kuwa kondomu hazihitajiki kutumika wakati wa kufanya mapenzi kinyume na maumbile. Hii ilihushishwa na ufahamu kuwa maambukizi ‘yapo tu kwenye sehemu zenye unyevunyevu (ukeni)’ na kwamba njia ya haja kubwa ‘hairuhusu matumizi ya kondomu’; kondomu inapunguza ‘ukavu’ na msugvano/raha wakati wa kufanya mapenzi na ‘inaweza kuzama ndani’.

Hitimisho

Washiriki katika utafiti huu walieleza mazoea na ufahamu wao juu ya kujamiiana kinyume na maumbile na kuonekana kuwa vinawaweka kwenye hatari kubwa ya kupata maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VUU) na magonjwa ya zinaa. Umakini mkubwa na waharaka wa kutoa elimu juu ya kujamiiana kwa njia ya haja kubwa unahitajika Tanzania, ambapo njia hii ya kujamiiana bado inachukuliwa kuwa ni ya kimila. Utafiti huu unatoa taarifa muhimu ambazo zinaweza zikajumuishwa kwenye mpango wa elimu ya kujamiiana.